**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 02 “Ndizi za majivu”**

**Author:** **Njoki C. Muhoho**

**Medical Advisor** **Dr. Ng’ethe Muhoho**

**Editor** **Maja Braun**

**Kisuaheli** **Eric Ponda**

| Scene | Characters | |
|---|---|---|
| **1** | 1. MAMA SAM<br>2. MARIA<br>3. CHEMU<br>4. NARRATOR | **SAM – 17, m.**<br><br>**MAMA SAM – 40, f.**<br><br>**MARIA – 43, f.**<br><br>**EDDI– 36, m.**<br><br>**DR SALLY – 34, f.**<br><br>**CHEMU – 15, f.**<br><br><br>**NARRATOR** |
| **2** | 1. MAMA SAM<br>2. MARIA<br>3. CHEMU<br>4. NARRATOR | |
| **3** | 1. SAM<br>2. CHEMU<br>**3.** MARIA<br>**4.** NARRATOR | |
| **4** | 1. MAMA SAM<br>2. MARIA<br>3. CHEMU<br>4. EDDI | |

**<u>INTRO</u>**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** **Hujambo na karibu kwa makala ya pili ya mfululizo wa vipindi vyetu vya LEARNING BY EAR, NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO, tukiangazia ugonjwa wa kuhara na madhara yake kwa mwanadamu. Katika makala iliyotangulia, Familia ya Sam inakumbwa na matatizo yanayosababishwa na ugonjwa huu wa Kuhara. Kadhalika Mama Sam anaahidi kuwatembelea shemeji yake Eddi na mkewe Sally ambao ni madaktari, ili kupata ushauri zaidi kuhusiana na maradhi haya. Je Mtoto wake Fatu atanusurika na janga hili au kuwa miongoni mwa Watoto wengi tu barani Afrika wanaofariki kutokana na ugonjwa wa Kuhara?**

Sikiliza ujifunze mengi kuhusu chanzo, tiba na hata kinga dhidi ya ugonjwa huu wa Kuhara,tunapoungana naye Sam, Familia yake na marafiki pia.

**<u>SCENE 1: MAMA SAM'S HOUSEHOLD</u>**

**02. SFX: BABY CRYING IN BACKGROUND, KNOCK ON THE DOOR**

**03. MAMA SAM :** ***(harassed)*** Pita ndani….. mlango uko wazi.

**04. MARIA :** Habari za asubuhi Mama Sam. Ohh Usiniambie Mtoto wako bado analia. Huyu mtoto Fatu kweli anapumzi nimemsikia akilia nikiwa huko barabarani.

**05. MAMA SAM :** Habari za asubuhi Maria, nina wasi wasi, na ni wakati kama huu ninapo mkumbuka marehemu mume

wangu. Angekuwa hai tayari angejua kinachowasumbua wanangu

**06. MARIA :** Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi na namlani dereva aliyesababisha ajali hiyo iliyomchukua Baba Sam. Mungu amrehemu…!, Mimi na wewe sasa lazima tutafute njia za kumtibu Fatu. Nimekuja na Chemu atusaidie,. …

**07.** ***SFX: BABY CRYING STOPS***

**08. CHEMU :** Mjomba Eddi na shangazi Sally wanakuja lini?

**09. MARIA :** ***(sternly)*** Chemu, njoo hapa, hebu nenda ukawakishe moto, namimi nichambue hizi ndizi. Inaonekana Fatu sasa amelala, na wakati atakapoamuka…., ndizi zitakuwa tayari.

**BRIDGE MUSIC**

**10. NARRATOR** Ndizi na Moto?. Maria anapanga njama fulani.Jee anafahamu anachofanya, kujaribu kutibu ugonjwa unaowaua watu wengi barani Afrika? Ni matumaini yetu kwamba atalifahamu hilo yaani athari za Ugonjwa huu. Endelea kutusikiliza..

**SCENE 2: MAMA SAM'S FRONT ROOM**

**11.** ***SFX: FIRE CRACKING. SCRATCHING OF DRY WOOD*.**

**12. MARIA :** Rafiki yangu Mama Sam…! hebu nikudokezee kuhusu mchanganyiko wa dawa hii ya kuhara. Ni

nzuri kuliko madawa ya kisasa..!. Chemu hakikisha huo moto unatoa jivu jingi kabisa.

**13. MAMA SAM :** Jivu?

**14. MARIA :** Ndio. Na likiwa bado moto kabisa Sasa chambua ndizi hizi mbichi kisha uzioke kwenye jivu hilo la moto. Hakikisha zinaiva kwenye hilo jivu.

**15. CHEMU :** Lakini ni ngumu sana, sasa tutawezaje kulifuta jivu zitakapoiva?

**16. MARIA :** Nani amezungumzia suala la jivu kufutwa. Na tena nani anayehitaji ndizi mbivu ukiwa unahara?Ndizi ngumu zilizo na jivu jingi ndiyo dawa nzuri ya tumbo!

**17. MAMA SAM ;** ***(horrified)*** Nzuri kwa nini? Sasa, Maria umeanza kunitia wasiwasi.

**18. CHEMU :** Nafikiri bora twende hospitalini sasa. Lazima twende!

**19. MAMA SAM :** CHEMU, Usitie shaka, Eddi atafika si kitambo na atatueleza cha kufanya. Yeye anafahamu barabara masuala ya afya.

**20. CHEMU :** ***(excited)*** Kwani Eddi anakuja leo? Vizuuurii,…. Vizuuri sana !

**21. MARIA :** Nyinyi wawili kipi msichokifahamu hapa? Fatu anahitaji kula ndizi hizi zilizotiwa jivu.Ndizi hizo ngumu na jivu zitazifanya sehemu za ndani za utumbo wake kuwa ngumu na hivyo kuzuia kuhara.Hiyo ndiyo dawa ya ugonjwa wa kuhara mahsusi kwa familia hii.Sasa ni nini ambacho hujakielewa?

**22. CHEMU :** ***(in sotto voice)*** Mimi nina wasiwasi. Uko wapi Eddi jamani? ***(loudly)*** Sam yuko wapi!

**23. MAMA SAM Chumbani mwake.amedhoofika kiafya.siku hizi anapenda kulala kila wakati.!.**

**24. CHEMU : Wacha nikamuone.**

**25. MARIA : (*shouting)* Usiende.!, wasichana wenye tabia nzuri hawapaswi kuingia vyumbani mwa wavulana**

**26.** ***SFX: DOOR SLAMS***

**27. MARIA :** Nimechelewa. ***(muttering to herself)*** Lakini hawa watoto wanatusikiliza siku hizi..sidhani..!

**BRIDGE MUSIC**

**<u>SCENE 3: SAM'S BEDROOM</u>**

**28. CHEMU :** Sam, Sam, Umeamka? Wajisikiaje na hali yako sasa?

**29. SAM :** ***(weakly)*** Nafuu kidogo, japo najisikia mdhaifu.

**30. CHEMU :** Poleee….! waonekana mdhaifu kweli

**31. SAM :** ***(sarcastic)*** Hmm…...nishapoa!

**32. CHEMU ;** ***(coyly)*** Pole Sam, sikutaka kukuudhi. Pole sana kwa ugonjwa…. Ungependa… ungependa nikusomee kitabu?

**33. SAM :** Ningependa sana…lakini .. hebu kwanza keti hapa tuzungumze

**PAUSE**

**34. CHEMU :** Au naweza kukuimbia wimbo?

**35. SAM :** Wewe? Haya imba kama unaweza!

**36. CHEMU ; Ehh naweza *kurap!* Tena *rap* nzuri sana** …!

**37. SAM :** *(**Laughs**) Rap* ya kuniongoa?, wimbo mzuri sana…! Ehhe ulijifunza wapi wimbo huu?

**38. CHEMU :** Huu wimbo nimekutungia wewe … ili kukusaidia kupambana na ugonjwa huu wa kuhara..

**39. SAM ;** Wimbo wenye una hisia za mahaba?

**40. CHEMU :** *(**chiding**)* Wacha ushari wako ! , huu ni wimbo wa kukusaidia kujikinga na Ugonjwa huu.utapona….!

*Wash your hands - Osha mikono yako , Osha mikono yako.*
*Only washed hands- Mikono safi tu hutumiwa kwa kula*

*Should be used*
*To eat*
*Only careless people Watu wasio jali tu hutumia mikono michafu.Baada ya msala, Osha mikono yako.Dumisha afya yako,Osha mikono yako.*
*Use unwashed hands*
*After visiting the toilet*
*Keep healthy*
*Wash your hands.*

**41. MARIA (V O)** ***(Very loud shout from outside the room)*** Chemu,toka hapa nje upesi! Chumba cha Sam si studio ya kurekodi muziki. Toka nje kuna kazi inakusubiri huku, na nakuhesabia… moja… mbili…

**42. NARRATOR Haya basi Mama hapendi kusikia mambo ya *Rap*.Lakini cha msingi kwa Chemu ilikuwa tu kupata nafasi ya**

**kumuona Sam akitabasamu japo kidogo tu. Na wakati huo huo ndizi bado zinaendelea kuiva jikoni.**

**SCENE 4: MAMA SAM'S FRONT ROOM**

**43.** ***SFX: BABY FATU IS CRYING AGAIN***

**44. MARIA :** Kusema na kweli huyo mototo wako anapumzi za kulia ...! Lakini subiri hadi atakapo kula hizi ndizi, atanyamaza kimya … kama… mototo… mwenye afya nzuri.

**45.** ***SFX: (HEARD FROM INSIDE MAMA SAM'S HOUSE) - SOUND OF CAR DRIVING UP. CAR PARKS***

**46. MAMA SAM :** ***(excited)*** Eddi amefika,gari lake lile.…!

**47. CHEMU :** (***excited***) Ni yeye,… ni yeye…. mjomba Eddi amefika.!

**48.** ***SFX: DOOR OPENS. BABY FATU CONTINUES CRYING***

**49. EDDI :** Hamjambo nyote…! Kwanini mototo analia? … hiyo harufu mbaya hapa ni ya nini?

**50. CHEMU :** ***(excited)*** Mjomba Eddi, afadhali umefika…!, Fatu ni mgonjwa sana!. Sam naye hawezi tena kukimbia kwasababu tumbo lake limekuwa likimsumbua. Kwa sasa amelala tukisubiri ndizi ziive..

**51. EDDI ;** ***(confused)*** Eeeh?

**52. MAMA SAM** Eddi, Shemeji yangu umefanya vizuri sana kuja kutuona.

**53. MARIA :** ***(sarcastic)*** Bw Eddi hatimaye umefika...!

**54. EDDI :** Nafurahi kuwaona Maria… Mama Sam, kwanini Fatu analia hivi? Hebu nimuone!

**PAUSE**

**55. EDDI ;** Oh hapana …hapana.. huyu mtoto ni mgonjwa sana. Mama Sam huyu mtoto anapaswa kupelekwa hospitalini mara moja ..!. Hebu mtazame, mwili wake umedhofika, amepoteza maji yote mwilini. Hata amekuwa mdogo. Mara ya mwisho kumuona ilikuwa lini vile? Miezi miwl iliyopita? …. Kwani ameacha kukua au vipi?

**56. MARIA :** ***(stubbornly)* Sikiliza nikwambie Eddi, sihitaji msomi kama wewe kuelezwa kwamba maumbile ya Fatu ni kama ya wazazi wake*.* *(sarcastic)*…** Aliacha kukua. Hebu mtazame Mama Sam,…. ni mfupi kama nyundo. Hata Baba Sam, Mungu amrehemu, hakuwa mrefu vile….!Sasa unataka Fatu awe mrefu afanane na nani?. Ni umbile la ukoo sio ugonjwa.'

**57. CHEMU ;** *(**smugly**)* Anahara mjomba Eddi. Mimi nimekuwa nikiwaambia muda wote huu

**58. MARIA :** **M**toto wa kike taratibu!.

**59. EDDIE : Amekuwa akihara kwa muda gani**?

**60. CHEMU ; Kwa muda wa siku kadhaa sasa, lakini tunatayarisha ndizi…….**

**61. MARIA :** Nimesema Nyamaza msichana.

**62. EDDIE ;** *(**livid mad**)* Ndizi? Ndizi zitasaidia nini katika hali hii mbaya? Hebu tumpeleke hospitalini mara moja……, sasa hivi twendeni……! *(**softly**),* Mungu, natumai hatujachelewa.

**63. MAMA SAM ;** ***(worried)*** Ah jamani, kwani nimemfanya nini mwanangu?

**64. EDDIE : Ugonjwa wa kuhara ni mbaya sana. Huua. Fatu alipaswa kumuona daktari mapema katika kipindi cha siku saba za mwanzo. Mtoto anapoanza kuhara, hudhoofika na kupoteza maji yote mwilini katika muda wa masaa machache tu… na.. na sitaki kusema zaidi…Mama Sam ingia garini mwangu sasa hivi twende Hospitalini..fanya upesi…!**

**65.** ***SFX: RUFFLE AND SHUFFLE OF CLOTHING AND FOOTWORK***

**66. CHEMU Pia mimi ningependa kuandamana na nyinyi mjomba Eddi!**

**67.** ***SFX; DOOR OPENS, FOOTWORK, DOOR SHUTS. CAR ZOOMS OFF IN RUSH. (All sound heard from indoors)***

**SILENCE**.

**68. MARIA : Na nani atakula hizi ndizi za kuchoma ?**

**OUTRO: NARRATOR** Hali ya Mtoto Fatu inazidi kuwa mbaya sana. Ugonjwa wa kuhara haukupata tiba mapema, na kuna hatari huenda Mtoto huyu Fatu akafariki kama wengine wengi wanaofariki barani Afrika kutokana na kuhara,kwasababu wanayapuuza madhara ya ugonjwa huu. Ungana nasi tena kwa makala yajayo ya Noa Bongo Jenga maisha yako ufahamu kitakachojiri katika mfululizo wa mchezo huu wa kuigiza. Hatma ya Sam bado anayeugua kitandani ni ipi ..Je Ni nani anayemsaidia chumbani mwake? . Pia unaweza kuutazamaa mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe ili ufahamu mengi zaidi kuhusu vipindi hivi vya Noa Bongo au kututumia maoni yako. Hadi wakati mwengine kwa heri kwa sasa!